**TAARIFA YA MAHITAJI KWA MWANACHUO MWAKA 2025**

**MAHITAJI ANAYOTAKIWA KUJA NAYO NI:**

| NA | KIPENGERE | MWAKA WA I, 2024 |
|---|---|---|
| 1 | **ADA YA MWAKA HUU** | **60,000** |
| 2 | BEJI | 3,000 |
| 3 | KITAMBULISHO | 4,000 |
| 4 | MICHEZO | 10,000 |
| 5 | FULANA (TSHIRT) | 16,000 |
| 6 | MAHAFALI YA MWISHO | 15,000 |
| 7 | *BIMA YA AFYA* | *50,400* |
| 8 | *SURUALI* | *32,000* |
| 9 | *OVERALL/OVERCOAT* | *30,000* |
| | **JUMLA YA LIMBIKIZO** | **220,400** |

***KUMBUKA.*** *MALIPO YOTE TAFANYIKA MARA BAADA YA KUFIKA CHUONI NA KUPEWA NAMBA YA MALIPO YA SERIKALI GePG (**"Control Number"**) TOKA KWA MUHASIBU WA CHUO*

Kila Mwanachuo anatakiwa **LAZIMA** awe na vifaa vifuatavyo pindi arejeapo Chuoni:

1. Kitambulisho ama namba ya **NIDA** *(kama una umri wa miaka 18 au Zaidi)*
2. Jozi mbili za viatu vyeusi ***vya Kamba*** kwa ajili ya siku za masomo ya kawaida.
3. Jozi moja ya viatu vya **USALAMA** (Safety Boot) kwa ajili ya siku ya "practical"
4. Vifaa vya hesabu (Mathematical Set)
5. Sweta rangi ya Bluu ***(sweta za shule)***
6. Soksi nyeusi jozi mbili
7. Shati nyeupe mbili za mikono mifupi aina ya tomato.
8. Suruali overlall na overcoat ***LAZIMA*** zishonwe chuoni kwa gharama ya mzazi.
9. Mwanafunzi atatakiwa kuja na fyekeo, ufagio wa chelewa ***(mkubwa)*** pamoja na rim moja ya karatasi ***(Double A)*** na ***si vinginevyo*** kwa kila mhula.
10. Bima ya Afya ni lazima kila mwanachuo kuwa nayo, hivyo mwanafunzi asiye na Bima hatapokelewa chuoni.

**NB:**

1. Gharama za kujikimu kipindi chote cha mafunzo kwa vitendo ni mchango wa mzazi. Hivyo mzazi unashauriwa kufanya maandalizi mapema
2. Kila mwanachuo alipie hela ya mtihani wa mwisho (CBA) muhula wa kwanza pindi anaporipoti Chuoni ili kuepusha usumbufu.
3. Malipo ya ***ADA*** pekee yatafanyika kwa awamu moja au mbili, Michango mingine yote italipwa kwa mara moja mwanzoni mwa muhula wa kwanza 2025. Malipo yote yafanyike kwa ***"Control Number"*** atakayoipata Chuoni na si mahala kwingine. ***Zingatia hili.***

MKUU WA CHUO
VETA - MARA
S. L. P 188
MUSOMA

Martin S. Mollel

**Mkuu wa Chuo - VETA Mara**

**VOCATIONAL EDUCATION AND TRAINING AUTHORITY (VETA)**

The Medical Officer                                        Date:..............................

..............................................................................
..............................................................................
..............................................................................
..............................................................................

**REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION TO:**........................................................
Please examine the above named candidate to his/her fitness to undergo training and subsequently work as a/an

(i) Eyesight.................................................................. (ii) Hearing........................................

(iii) Asthma ......................................................................

(iv) Other serious diseases ......................................................................

**Medical Certificate:**

I have examined the above named and consider that he/she is physically fit/unfit for training as above

*Date:*......................*Designation*..............................*Signature & Official Stamp*...........

........................................................................................................................................................

**KUKUBALI NAFASI YA MAFUNZO YA UFUNDI STADI:**

**(a) MWANACHUO:**

Mimi.......................................................... ninakubali nafasi ya mafunzo katika fani niliyopangiwa, pamoja na kuzingatia sheria na kanuni za chuo.

*Sahihi*..................................................................... *Tarehe*...................................................

**(b) MDHAMINI:**

Mimi..................................................................... wa S.L.P...................................................................
Ninathibitisha kuwa ninamdhamini aliyetajwa hapo juu na nitamlipia gharama zote za mafunzo (ada) n.k. pamoja na nauli na gharama zote wakati wa kwenda chuoni, na wakati wa kwenda kwenye mafunzo viwandani (Field Attachment) na kurudi nyumbani wakati wa likizo na baada ya mafunzo.

*Sahihi*..................................................................... *Tarehe*...................................................

## SHERIA ZA CHUO KWA WANAFUNZI WA KUTWA

**ILI KUFANIKISHA MAFUNZO YA AWALI YA UFUNDI KILA MWANACHUO ANATAKIWA KUFUATA SHERIA ZIFUATAZO:-**

### 1. MAHUDHURIO:

(a) Kila mwanachuo anatakiwa kufika chuoni kuanzia saa 1.15 asubuhi. Hii ina maana ifikapo saa 1.30 wanachuo wote wawe wameshafika chuoni, wakiendelea na usafi wa mazingirana ndani na nje ya karakana. Kuishi mbali siyo sababu wala udhuru wa kuchelewa ***Adhabu kali itatolewa kwa wachelewaji***.

(b) Mwanachuo haruhusiwi kutoka nje ya chuo kwenda nyumbani, hospitali au sehemu nyingine yoyote ile bila kuruhusiwa na mwalimu *(Mkuu wa Sehemu)*

(c) Mwanachuo apatapo matatizo ya msiba, kuuguliwa au kuugua mwenyewe ni lazima habari zake zifike chuoni za kutoa taarifa hiyo bila ya kufanya hivyo ni kosa.

(d) Mahudhurio chini ya asilimia 85% mwanachuo atanyimwa cheti cha kuhitimu mafunzo

### 2. MAVAZI:

(a) Sare ya chuo ni suruali ya blue na shati jeupe la mikono mifupi. Sare hiyo ivaliwe wakati wote mwanachuo awapo chuoni na wakati wa safari ya kuja chuoni na kurudi nyumbani. ***Wakati wote shati liwe limechomekwa***.

(b) Ovaroll livaliwe wakati wa vipindi vya kazi za mikono tu.

(c) Viatu vyenye visigino virefu, kandambili au sandozi haviruhusiwi kuvaliwa chuoni

(d) Hairuhusiwi kwenda na sare ya chuo sehemu za starehe kama vile baa, sinema au sehemu zinazolingana na hizo.

### 3. USAFI WA MWILI:

(a) Hairuhusiwi kuvaa hereni, pete, bangili na mapambo ya aina yoyote ile kwa kipindi chote cha mafunzo:

(b) Hairuhusiwi kutumia vipodozi au manukato yanatoa harufu mbaya kiasi cha kusumbua wengine kufuata masomo.

(c) **Nywele kwa Wavulana:**

- (i) Zikatwe ziwe fupi na mitindo kama PANKY, AMERICAN BASE NA KIPARA hairuhusiwi kabisa.
- (ii) Ndevu haziruhusiwi kabisa.

(d) **Nywele kwa Wasichana:**

- (i) Zikatwe ziwe fupi au zisukwe kwa mstari (twende kilioni)

NB: Nywele ndefu na nywele zenye kupakwa madawa kama vile Carl, Raster, Golden Hair haziruhusiwi kabisa kwa kipindi chote cha mafunzo.

4. **WIZI WA MALI ZA CHUO AU MALI YA MTU YOYOTE YULE:**

(a) Vitendo vyote vya wizi haviruhusiwi. Pindi ikibainika mwanachuo ameiba mali ya chuo au ya mwanachuo mwenzake, basi atafukuzwa chuo mara moja.

(b) Ukipoteza vifaa vya chuo utatakiwa kulipa gharama kamili ya kifaa au ukakinunue kifaa chenyewe au ukilete badala ya ulichopoteza.

(c) hairuhusiwi mwanachuo kuingia na kifaa chochote kile kinachofanana na vile vilivyoko ndani ya chuo.

(d) Mwanachuo atapekuliwa wakati wa kutoka karakana na wakati wa kutoka getini

5. **UGOMVI:**

Ugomvi, kupigana au kushambuliana ni makosa ya jinai. Atakayepatikana akijihusisha na matendo ya namna hiyo atafukuzwa chuoni na kukabidhiwa kwenye vyombo vya dola.

6. **ULEVI:**

Iwapo itabainika mwanachuo analewa, au kuonekana katika sehemu za vileo, anavuta bangi au madawa ya kulevya adhabu yake ni kufukuzwa chuo mara moja.

7. **MAPENZI:**

(a) Uhusiano wa kimapenzi chuoni kati ya mwanachuo na mwanachuo au kati ya mfanyakazi na mwanachuo hauruhusiwi kabisa.

(b) Mwanachuo akiwa na mimba hataruhusiwa kuendelea na masomo.

(c) Mwanachuo wa kiume au wa kike haruhusiwi kuingia maeneo wanayoishi watumishi bila ya kibali au ruhusa.

8. **MIGOMO:**

Migomo ni marufuku, au kuchochea migomo ni kosa lisilostahimilika. Atakayeshawishi au kusababisha migomo atafukuzwa chuoni mara moja.

9. **LUGHA:**

Lugha inayotumika kuendeshea masomo ni kiingereza hivyo ni wajibu wa kila mwanachuo kujifunza kiingereza.

10. **JINA:**

Jina lisibadilishwe mpaka ziwepo sababu na hati maalum kwa uthibitisho na ajulishwe Mkuu wa Chuo mara moja.

11. **WAKATI WA MASOMO MWANACHUO HARUHUSIWI:-**

(a) Kuvaa bangili, kukali nywele, kupaka rangi ya mdomo na kucha, na kupaka wanja.

(b) Kuvaa kandambili (sandals) ziwe za mpira au tyre, viatu vyenye visigino virefu (raison)

(c) Ovaroli livaliwe kwenye karakana tu na wala sio darasani.

Martin S. Mollel

**Mkuu wa Chuo - VETA Mara**

MKUU WA CHUO
VETA - MARA
S.L.P 188
MUSOMA